**Sikiliza na Ujifunze - Mazingira na Hali ya Hewa**
**03 – Bushmeat (Nyamapori)**
**Text : Richard Lough**
**Redaktion und Idee: Johannes Beck**
**Translator : Mohamed Dahman**

---

Hujambo msikilizaji! Karibu katika mfululizo wa vipindi maalum juu ya masuala ya mazingira. Katika kipindi cha leo tutazungumzia juu ya athari za harakati za binaadamu kwa wanyama barani Afrika. Misitu ya joto na uwanda mpana wa miti ya hapa na pale barani Afrika ni maskani ya wanyama na viumbe hai aina mbali mbali. Lakini tamaa kubwa ya binaadamu kwa mali asili ya bara hilo husababisha kupungua kwa idadi ya wanyama hao. Radionovela leo itawaeleza juu ya taathira mbaya ya biashara haramu ya nyamapori ambayo inaendelea kushamiri barani kote Afrika na ni wanyama gani walioko hatarini kabisa.

Kadhalika mwandishi wetu wa Kenya Richard Lough (anatamkwa Lock) atatufahamisha kwa nini ni muhimu kuzingatiwa kwa suala la kupotea kusikorekebishika kwa mfumo wa maisha ya kutegemeana ya wanyama na mimea.

**Music – 0:30**

**Radionovela**

**SFX – Sitting down at desks …….Kuketi kwenye vidawati**

**Alice:** Habari za mchana! Hamjambo wanafunzi.

**Moses, Gladys, Monica:** Hatujambo!

**Alice:** Jina langu ni Alice Lubega, nafanya kazi na shirika linaloitwa Fighting Bushmeat la kupiga vita uuzaji wa nyamapori. Nimekuja shuleni kwenu leo hii kuzungumza nanyi juu ya umuhimu wa kutunza wanyama pori. Je nani amewahi kuona wanyama pori?

***(collective hands go up in the air with a yes miss'……mikono inainuliwa hewani kuashiria kuwa wameona na sauti ya ndio )***

**Alice:** Naam! Wewe….

**Moses:** Ndiyo Bi. Alice, jina langu ni Moses. Napenda wanyama pori lakini mara nyingi wakati wa usiku tembo wanakuja kwenye shamba letu na kula mazao yetu. Mwezi uliopita waliharibu mavuno yetu yote ya mahindi.Walisababisha uharibifu mkubwa na ilibidi tuwafukuzie mbali.

**Alice:** Enhe! Moses unapenda wanyama gani wengine?

**Moses:** Napenda pundamilia na chui. Nikiwa mkubwa nataka kuwa askari wa mbuga kusaidia kutunza wanyamapori.

**SFX –hand clap ….makofi yanapigwa**

**Alice:** Vizuri sana.

**Moses:** Pia nimewahi kuona paa wengi ambao huwawinda pamoja na kaka zangu.

**Alice:** (*exclaim ……tamka kwa mshangao* ) Ohhh!

**Moses:** Ndiyo, huwa tunawasaka na mbwa wetu na mara nyingine huweka mitego.

**Monica**: Kwa nini mnafanya hivyo Moses?

**Moses:** Siku nyingine huwa tunakula nyama zao. Unajua wiki hii tulimnasa kima katika mojawapo ya mitego yetu. Tulimla kima huyo na nyama yake ni tamuuuu...

**Monica:** (*frustrated sigh…..guno la kukata tamaa*) Hmmmm ….lakini Moses huwezi kusema kwamba unapenda wanyama pori na unataka kuwa askari wa mbuga wakati huo huo unasema unafurahia kumla kima…

**Moses:** Lakini hakuna mtu aliyewahi kuniambia kwamba kufanya hivyo sio halali. Wakati mwingine huwa hata tunakutana na askari tukiwa tumebeba mizoga yao. Katu hawajawahi kutusimamisha.

**Alice:** Moses sina budi kukwambia kwamba kile unachofanya ni kinyume na sheria.

**Moses:** Lakini nakumbuka kuwinda na babu yangu nikiwa na umri wa miaka mitano tu. Huwa tunamnyemelea paa kwa nyuma na babu yangu huwauwa kwa upinde na mshale…

**Alice:** Ni kweli Moses mababu zetu walikuwa wakiwinda wanyamapori kwa ajili ya chakula. Lakini tatizo ni kwamba sasa magenge ya ujangili huwawinda paa wetu, kima na hata sokwe. Magenge haya huwinda katika kiwango cha biashara.

**Gladys:** Unamaanisha kwamba wanauza nyama?

**Alice:** Ndiyo hasa. Naam hebu twendeni mjini…

**SFX – road traffic …sauti ya magari barabarani**

**Alice:** Miaka miwili iliyopita, shirika letu lilifanya uchunguzi. Tuligundua kwamba asilimia 20 ya nyama iliyopatikana kwenye maduka ya kuuza nyama katika mji wetu ilikuwa ni nyamapori.

**Gladys:** Nyamapori ni nyama gani?

**Alice:** Tunaielezea nyampori kuwa ni nyama inayotokana na wanyamapori wanaoishi katika misitu na mbuga zetu.

**Moses:** Ikiwa ni pamoja na kima?

**Alice:** Wakiwemo kima.

**Monica:** (*gasps of horror .....duwao la mshtuko*) Hilo ni jambo baya. Vipi wanafanya hivyo wakati sio halali?

**Alice:** Kwa sababu huwa hawaiuzi kama ni nyamapori na badala yake huwa wanaiuza kama ni nyama ya ng'ombe au mbuzi. Lakini kwa kweli huwa ni nyama ya paa au pundamilia au hata nyati.

**Gladys:** Kwa hiyo watu wananua nyamapori bila ya kujua ?

**Alice:** Hapana hatudhani kwamba hawajui. Kutokana na uchunguzi wetu imebainika kwamba watu wananua nyampori kwa makusudi. Unajua barani Afrika nyamapori inaonekana kama kitu fulani kizuri. Hata Waafrika wanaoishi nje bado wanafurahia ladha ya nyamapori juu ya kwamba wanajua kuwa kwa kula nyama hiyo wanahatarisha idadi ya wanyamapori.

**Gladys:** Wanajua?

**Alice:** Kusema kweli wanajua.

**Monica:** Mchana huu hatuna budi kuutumia na kaka yangu Simon yeye ni askari wa mbuga katika Mbuga yetu ya Taifa.

**X-fade from SFX –road trafic to SFX 4x4 Safari vehicle .. changanya sauti ya magari barabarani na sauti ya gari la 4 wheel**

**Simon:** Majangili wana mitego isiyo stadi kabisa lakini ya kikatili inayofanya kazi kisawasawa kunasa mawindo yao.

**Gladys:** Ndiyo Moses anaweza kukuelezea juu ya mitego hiyo yote.

**Simon:** Sina haja ya mimi kujua. Na kama hayo wanayosema ni kweli Moses basi nataka usikilize kile nitakachosema.

**Moses:** Ndiyo bwana…

**Simon:** Ujangili katika sehemu hii umezagaa sana. Kwa kweli umezagaa nchi nzima.Unajua kwamba inakadiriwa katika miaka 30 iliyopita tumepoteza takriban theluthi mbili ya wanyamapori wetu.

**Moses:** Dohhh… na wote kutokana na ujangili?

**Simon:** Sio wote… wakati idadi ya watu wetu inaongezeka wanyamapori wetu wanazidi kukabiliwa na ushindani wa kuwania ardhi, jambo ambalo linaathiri idadi yao. Lakini uko sawa kuwinda kwa ajili ya nyamapori ni sababu kuu ya kupungua kwa idadi ya wanyamapori.

**SFX – slowing down vehicle …..kupunguza mwendo wa gari**

**Simon:** Angalia… unaona wale tai wanaozunguka angani? Mara nyingi utakuta kuna mzoga karibu na hapo. Hebu tuangalie huenda akawa mnyama alienaswa na mtego.

**SFX – open vehicle doors ….funguwa milango ya gari.**

**Monica:** Sina hakika iwapo nataka kuona jambo hili…

**SFX – vehicle doors close…….funga milango ya gari ………**
**SFX – walking through grasses ….tembea kwenye nyasi**

**Simon:** Hivi sasa tuna timu iliopewa majukumu ya kupambana na majangili. Kila wiki hugundua mamia ya mitego. Mengine imetegwa kwa ajili ya wanyama wadogo kama vile nungu na mengine kwa ajili ya wanyama wakubwa kama pundamilia.

**Gladys:** (*squeal ….toa sauti kali* ) Ahh …hapana…..

**Simon:** Hiki ndicho tunachokiona kila siku. Huyu ni diki diki mojawapo wa paa mdogo kabisa huyu ana urefu wa kama cm 30 lakini tayari amekamilika kuwa mkubwa. Katika

miaka michache ijayo kutakuwepo na paa wachache wa jamii hii.

**Gladys:** Ni wanyama wa aina gani walioko hatarini kabisa kutoweka?

**Simon:** Ah, inategemea unazungumzia nchi gani. Hapa ni paa kama vile diki diki, swalapala na pia tandala. Hebu tumchukue diki diki huyu.

**SFX – walking through grasses …kutembea kwenye nyasi**

**Gladys:** Na mahala gani pengine kuna ujangili?

**Monica:** Nimesikia kwamba katika misitu ya joto barani Afrika majangili wanawaua masokwe kufikia kiwango cha kutoweka.

**Simon:** Hiyo ni kweli. Katika baadhi ya sehemu za bara hili majangili wanawaangamiza masokwe. Kuuwawa kwao kumetangazwa sana na vyombo vya habari lakini taathira ya ujangili hata hapa ni mbaya. Karibuni tutakuwa na wanyama wachache tu wa kuwalinda na jambo hilo litaathiri uchumi kwa vile watalii watatafuta sehemu nyingine za kwenda.

**Moses:** Kwa hiyo vipi mnaweza kuzuia ujangili ?

**Simon:** Kwanza hebu niache nikuulize wewe Moses: Kwa nini watu wanafanya ujangili?

**Moses:** Mambo mawili aidha kwa chakula au kwa kuuza…

**Simon:** Sawa kabisa! Watu wengi wanaoishi karibu na mbuga zetu za taifa hawafaidiki kifedha kutokana na wanyamapori au watalii wanaokuja kuwaangalia wanyama hao kwa hiyo wanyama wanakuwa hawana thamani kwao. Unafikiri iwapo jamii hapa zingelikuwa zinafaidika kutokana na

mapato ya utalii wangewaangamiza wanyama ambao watalii wamekuja kuwaona?

**Monica:** Hawangelifanya hivyo. Lakini pia wanyama hawa ni sawa na vito vya thamani kwa bara letu. Angalia masokwe hivi sasa ni wanyama wanaotishiwa kutoweka katika uso wa dunia na mara watakapokuwa wametoweka hapo tena hawatokuwepo milele.

**Moses:** Je tayari tumechelewa sana kuwaokowa wanyama hao wanaotishiwa kutoweka duniani?

**Simon:** Hatukuchelewa. Unajua kwamba majangili walikuwa karibu kabisa wawatokomeze tembo wetu miongo miwili iliopita. Hivi sasa idadi yao ni kubwa… lakini inabidi tubadili tabia… inabidi tuwafanye watu wathamini wanyamapori wetu.

**Moses:** Naam sitokula tena nyamapori… sitokula tena kima! Kitoweo changu kitakuwa nyama ya ng'ombe na mbuzi tu!

***(Collective laughter ……..,…..Kicheko cha pamoja )***

**Music – 0:30**

**Je ulikuwa ukijuwa ?**

Je ulikuwa ukijua kwamba tishio kubwa kabisa la wanyamapori barani Afrika ni binaadamu? Tuchukulie mfano Kenya ambapo idadi ya wanyamapori imepungua kwa hadi asilimia sitini katika kipindi cha miaka thelathini tu. Mwendo kama huo uko barani kote Afrika. Wataalamu wanaamini kwamba kuna masokwe wasiozidi 110,000 barani Afrika. Ukilinganisha idadi hiyo na miaka mia moja iliopita inaaminika kwamba kulikuwako na masokwe zaidi ya milioni mbili wakining'inia kwenye misitu.

Kuna sababu kuu mbali mbali za mwenendo huo wa kutisha na kama tulivyosikia hivi punde biashara haramu ya nyamapori ni mojawapo

ya sababu. Kwa mujibu wa shirika moja la wanyamapori zaidi ya tani milioni 100 za nyamapori huchukuliwa kila mwaka kutoka misitu ya Bonde la Congo. Sababu nyingine ni kuongezeka sana kwa idadi ya watu barani Afrika. Kuna mshindi mmoja tu katika mashindano ya kuwania ardhi kati ya binaadamu na wanyama na mshindi huyo sio mwengime bali ni binaadamu. Kila siku tunaagamiza makaazi ya asili ya wanyamapori wetu na kufanya idadi yao izidi kupunguwa sana. Je jambo hilo linapaswa kuzingatiwa? Jibu bila ya shaka ndio! Kile tunachofanya ni kuuwa tu maisha ya kutegemeana kati ya viumbe na wanyama hayo ni maisha ya viumbe hai wa aina mbali mbali ndani ya mfumo wa ekolojia. Mfumo wa maisha hayo mara nyingi hutumika kama kipimo cha afya ya dunia. Mfumo wa maisha hayo ya kutegemeana ya viumbe hai kati ya wanyama na mimea haukugawika sawa sawa duniani kwa kweli hakuna mahala duniani penye maisha ya viumbe hai wengi aina mbali mbali kuliko kwenye misitu ya joto kunakopita mstari wa eqweta likiwemo bara la Afrika.

Mfumo huo wa maisha ulioko duniani leo hii wa viumbe hai kutegemeana ni matokeo ya mageuko kutoka sahili kuwa tata ya miaka bilioni nne. Hadi miaka milioni 600 iliopita ambapo kwa wastani ni kipindi kifupi cha maisha ya dunia maisha yote yalikuwa ni ya bakteria na viumbe hai wenye seli moja au chembe moja ya uhai. Lakini katika kipindi cha miongo michachae tu harakati za binaadamu zimewaweka maelfu ya wanyama na mimea kwenye orodha ya viumbe hai wanaotishiwa kutoweka katika uso wa dunia. Kubwa zaidi kupunguwa kwa maisha ya kutegemeana baina ya viumbe hai kwenye mfumo wa ekolojia kunaathiri chakula na afya ya watu wenyeji wanaoetegemea idadi kubwa ya wanyama, mboga mboga na aina ya mimea kwa ajili ya chakula na madawa. Ni vigumu sana kuweka idadi juu ya kupotea kwa mfumo huo wa maisha lakini hali hiyo haiwezi kurudi tena. Jamii ya viumbe hai ya wanyama na mimea iliotoweka katu haiwezi kujitokeza tena.

Lakini ukweli wa kuhuzunisha ni kwamba kiwango ambacho kwayo viumbe hai wanatoweka kinaongezeka sana.

**Outro …..Funga kipindi**

Na hapo ndio tumefikia mwisho wa mfululizo wa vipindi vyetu maalum vya Sikiliza na Ujifunze. Leo tulilenga juu ya mfumo wa maisha ya viumbe hai kutegemeana kati ya wanyama na mimea na biashara haramu ya nyamapori. Kwa hiyo kumbuka kwamba harakati au vitendo vyetu vina taathira ya moja kwa moja kwa makaazi ya asili ya wanyamapori wa bara letu la Afrika. Iwapo hatutowatunza hivi sasa itakuwa tumechelewa mno kuokowa viumbe hai fulani wanyama au mimea kutoweka duniani katika miaka inayokuja.
Asante kwa kuwa nasi iwapo unataka kukisikiliza tena kipindi hiki au kuwasimulia marafiki zako nenda kwenye mtandao wetu www.dw-world.de/be.
Kwaheri.